

Nimefurahi kuwa hapa leo. Sijawahi kufika hapa Mseroe ingawa kikundi cha Wazungu chini ya Village Education Project (Kilimanjaro) kilikuja kufanya kazi.

Leo ni nafasi kuwatakia wanafunzi wa darasa la saba kila la heri. Kila la heri kwa mitihani wiki ya kesho kutwa, na pia kila la heri kwa maisha yao ya baadaye.

Nataka kuchukua nafasi kuongea juu ya vikundi vinne. Cha kwanza kuna wanafunzi ambao wanafahamu au wanaotegemea kwenda sekondari; cha pili kuna wao wanaotegemea kwenda kusoma ufundii; cha tatu kuna wao ambao inawezekana watabaki nyumbani; na cha mwisho kuna wazazi wa hawa wa darasa la saba.

Nyinyi mtakaokwenda kusoma sekondari, au mtakaotegemea kwenda sekondari mtakuwa na bahati kuweza kuendelea na elimu yenu. Lakini fahamu, ukipata nafasi, kuna wanafunzi kumi ambao hawajapata nafasi. Siku hizi kwa kila nafasi kuna sio chini wanafunzi kumi na mmoja kushindania nafasi ile. Ukipata nafasi utakuwa na madaraka kusoma kwa bidii – vinginevyo umenyima wenzako kumi nafasi kusoma na umepoteza nafasi ile.

Nyinyi ambao hamtakwenda sekondari lakini mtakwenda shule ya ufundii, pia mtakuwa na bahati kuweza kuendelea na elimu yenu, hata kama ni elimu kupata ufundii maalum na sio elimu ya kitabuni. Mkisoma vizuri na kujitahidi mnaweza kushinda vyema na mwisho mtaweza kuanza na maisha mazuri na kupanga mnavyotaka.

Kwa hiyo, nyinyi mtakaoendelea kusoma shulenii hamtakosa maisha mazuri mkifanya kazi kubwa. Kwa hiyo ni juu yenu – fanyeni kazi kwa bidii na kupata matokeo

Au chezeni na kupotea kila kitu.

Nyinyi mtakaobaki nyumbani – kwa sababu hamtapata nafasi sekondari au ufundii au kwa sababu wazazi, kwa sababu yoyote, hawatakupelekeni shulenii – nyinyi mtaweza kupata shida, lakini nakuombeni kutokukata tamaa.

Muhimu ni kujenga utaratibu na kufanya kazi – msikae ovyo. Ukiweza kupata shamba – hata dogo kabisa – bado utaweza, kwa mfano, kulima mboga (nyanya, michicha) chochote, au kufuga kuku. Ukiifanya hivyo utaweza kupata pesa – na ukilimbikiza pesa mwisho utakuwa na mfuko.

Mfuku huu labda hautaweza kulipa ada ya shule, lakini – niamini – ukionekana kujisaidia hivyo kuna watu watakaokusaidia. Ukionyesha lengo lenye nguvu kusoma mpaka umepata mfuko wako wa pesa, utapata msaada. Usikate tamaa.

Pia sio kulimbikiza pesa tu, lakini kuhifadhi jina lako na kujenga jina lako. Watu watakuufahamu.

Wakisikia jina la Rehema – Oh, yule mvivu, mkorofii anayekaa baa pale chini – je, watakuwa tayari kumsaidia? Hapana.

Lakini kama jina la Rehema ni – yule, msichana msafi anayelima kila siku na anayeaza mayai yake na pia sio yeye ambaye alisaidia kubeba mawe kujenga kanisa jipya? – Je, watakuwa tayari kumsaidia? Nafikiri watakuwa tayari.

Fahamu kwamba baada ya kumaliza shule ya msingi ni juu ya kila mmoja kujenga maisha na kujenga jina lake.

Mwisho, naingia hiki kikundi cha nne, wazazi.

Kila mzazi tangu huyu mtoto alizaliwa, umefahamu, umejua, atafika hatua hii. Umejua atakuwa na miaka kumi na mitatu au kumi na minne, na kumaliza kusoma shule ya msingi na kutegemea kuendelea kusoma. Kwa hiyo kila mzazi – umekuwa na miaka kumi na mitatu kupanga.

Kama hujapanga, na mtoto wako atakuwa mmoja kubaki nyumbani nafikiri unapaswa kujiuliza kwa nini uliamua kuwa na mtoto.

Mtoto kuachwa mwenye miaka kumi na mitatu au kumi na minne ni kitu cha aibu.

Baada ya kumaliza kusoma shule ya msingi kila mtoto yupo njia panda ya maisha yake.

Anahitaji uongozi kuweza kuchagua njia nzuri, kufuata njia ile na kutokupotea njia. Hizi sana sana ni kazi za wazazi. Mtoto kuambwiwa hakuna pesa kwa elimu yake sasa, hakuna mpango wa kupata kazi, kuna kukaa nyumbani tu, ni kumdharaau kweli. Mtoto anastahili kuthaminawa. Mwenye miaka kumi na mitatu au minne tu hajapata nafasi ya kujua maisha yake yatakavyokuwa, na bila kujua maisha yake yatakavyokuwa, je atakuwa na msaada gani kwa wazazi wake sasa au baadaye?

Kwa hiyo nawaombeni wazazi kufanya bidii kwa njia yoyote kuendelea kuelimisha watoto. Mimi nilisomeshwa tangu nilikuwa na miaka mitano mpaka nlikuwa na miaka ishirini na tatu, miaka kumi na minane ya elimu. Hata baada ya hii nimesoma kozi fupi tatu. Elimu haina mwisho – naomba kila mmoja hapa leo kutokufikiri kumaliza darasa la saba ni kumaliza kupata elimu. Ni msingi tu, na bado mna maisha ya kujenga.

Wanafunzi wa darasa la saba nawatakieni kila la heri kwa mitihani na kwa maisha ya baadaye, natumaini mtakumbuka Mseroe kuwa mahali pazuri mlipopata elimu ya msingi.

Asanteni